TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Agosti 28, 2015

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## Tamko kuhusu umuhimu wa kuendesha kampeni na mchakato wa uchaguzi mkuu kwa misingi ya haki, usawa na amani

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inapenda kuungana na wadau mbalimbali kukumbushia msimamo wake wa kuwaasa wadau mbalimbali katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ufanyike kwa haki, usawa na amani.

Tume imebaini kama walivyobaini wadau wengine kuwa kumeanza kujitokeza dalili zinazokiuka misingi hiyo.

Aidha, Tume inazishauri mamlaka zote - taasisi, vyombo vya dola, na watoa maamuzi mbalimbali kutenda haki na kuzingatia misingi ya **usawa** (equality), **uwazi** (transparency) na **kutobagua** (non-discrimination) katika utekelezaji wa majukumu yao ili kukuza haki za binadamu na kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

Tume inapenda kuwashauri viongozi wa vyama vya siasa, wafuasi wao, na wananchi kwa ujumla kujiepusha na mihemko ya kisiasa inayopelekea matumizi ya lugha za kejeli, ubaguzi na matusi katika kampeni za uchaguzi, ili kudumisha umoja, amani na utulivu uliodumu hapa nchini kwa miaka yote tangu nchi yetu ipate uhuru.

Kwa mujibu wa Kipengele cha 2.2(b) cha Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2015 yaliyosainiwa Julai 27, 2015 na vyama vya siasa, viongozi hao na wagombea wao wanatakiwa kujiepusha na matumizi ya lugha hizo zisizofaa.

Tume inapenda kuchukua fursa hii kutahadharisha na kukemea matumizi ya matusi na lugha zisizo na staha, katika kampeni zinazoendelea nchini za kunadi Ilani za Uchaguzi na wagombea wa urais, ubunge na udiwani, na kuwakumbusha wanasiasa na wafuasi wao kuzingatia maadili hayo ili kudumisha siasa safi, amani na utulivu nchini.

Tume inakumbusha kwamba mikutano ya hadhara ya kunadi sera, ilani na wagombea ni sehemu muhimu ya kutekeleza haki ya mwananchi ya kushiriki katika uongozi wa Taifa, ama moja kwa moja kama mgombea au kushiriki kumchagua mwakilishi wake.

Kwa hiyo ni muhimu mamlaka zihakikishe kunakuwepo usawa katika mchakato huo. Ni muhimu kuwepo na mazingira ya usawa *(level playing field)* ili zoezi la uchaguzi lipate uhalali *(legitimacy).*

Aidha, Tume inapenda kutahadharisha mamlaka, Vyama vya Siasa na Jeshi la Polisi kuhusu uwepo wa vikundi vya ulinzi ndani ya Vyama vya Siasa. Tume inasisitiza kwamba, uwepo wa vikundi hivyo ni kinyume na Katiba ya nchi.

Uzoefu unaonyesha kuwa katika nchi mbalimbali vikundi kama hivyo vimekuwa vyanzo vya vurugu na uvunjifu wa haki za binadamu, hasa wakati na baada ya uchaguzi mkuu kumalizika pasipokuwepo uwazi na haki. Vikundi hivi haviwajibiki kwa mujibu wa sheria kwa mtu yeyote, bali vinalinda maslahi ya vyama.

Kwa hivyo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inaitaka Serikali kupiga marufuku vikundi hivyo kujihusisha kwa namna yoyote ile katika mchakato wa uchaguzi, ikizingatiwa kwamba Jeshi la Polisi limeimarishwa kutoa ulinzi kwa wagombea, wananchi na mali zao.

Mwisho, Tume inaitaka Tume ya Uchaguzi kushughulikia kasoro zilizojitokeza wakati wa kuboresha Daftari la Wapiga Kura kwa kutumia BVR. Aidha, Tume inashauri kuwa wanafunzi wote waliojiandikisha wanapata fursa ya kupiga kura popote watakapokuwepo.

Tume imekuwa ikifuatilia kwa karibu mchakato wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kabla na baada ya ratiba za Vyama vya Siasa kuanza kampeni hapo Agosti 22, 2015 na kubaini mambo kadhaa yakiwemo matumizi ya lugha sizizofaa na ubaguzi, kutaja kwa uchache.

Imetolewa na:

Mhe. Bahame Tom Nyanduga
MWENYEKITI

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Agosti 28, 2015